TAASISI YA SAYANSI ZA AFYA MBALIZI

P.O BOX 6117
Mbeya
Tel. 025 2561022
Fax 025 2560348

P.O. BOX 6117
Mbeya
Tel. 025 2561023
Fax 025 2560348

Website :www.mbaliziinstitute.ac.tz Email :nursingmbalizi@yahoo.com

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI 10.01.2022

Taasisi ya Sanyasi za Afya Mbalizi ni Taasisi iliyopo katika Wilaya ya Mbeya (v) Mkoa wa Mbeya na inamilikiwa na Kanisa la Uinjilisti Tanzania iliyo na Makao Makuu yake katika mji mdogo wa Mbalizi Mkoani Mbeya. Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatayo;

(a) DAKTARI DARAJA LA II NAFASI 02 (NAFASI ZA KUJITOLEA).

(b) AFISA TABIBU NAFASI 02 (NAFASI ZA KUJITOLEA).

(c) UGAVI 01

(d) USAFI WA MAZINGIRA 03

(A) NAFASI ZA KAZI ZA UALIMU WA MAAFISA TATIBU (KUJITOLEA) 04, SHAHADA (MD) NAFASI 02 NA STASHAHADA (DIPLOMA) NAFASI 02.

1. Sifa za muombaji

- Awe amehitimu shahada/Stashahada ya Udaktari kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe amesajiriwa na Baraza la Udaktari Tanzania.
- Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu.
- Awe anajua kusoma, kuongea na kuandika lugha ya Kiingereza na Kiswahili.
- Awe anajua kutumia Computer; **Ms Word**, **Ms Excel, na Power Point.**

2. Kazi za Kufanya /Majukumu

- Kuwafundisha Wanafunzi wa kada ya Afisa tabibu.
- Kusimamia taratibu na sheria zilizowekwa na Taasisi na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.
- Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

3. MSHAHARA

- Kulingana na mwongozo wa serikali wa malipo ya kujitolea.

(B) AFISA UGAVI - NAFASI 01

1. Sifa za muombaji

- Stashahada ya Ugavi/ Ununuzi au Biashara iliyojiimarisha kwenye Ununuzi na Ugavi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali au sifa inalingana na hiyo inayotambuliwa na Bodi ya Wataalamu wa Ugavi na Ununuzi nchini.
- Awe amesajiliwa na PSPTB kama 'Procurement and Supplies Technician au 'Procurement and Supplies Full Technician'.
- Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu.
- Awe anajua kusoma, kuongea na kuandika lugha ya Kiingereza na Kiswahili.
- Awe ana ujuzi wa kutumia Kompyuta; **Ms Word**, **Ms Excel, na Power Point.**

2. Kazi za Kufanya /Majukumu

- Kutunza na kupanga vifaa vilivyomo ghalani katika hali ya usafi na usalama.
- Kupokea vifaa vilivyonunuliwa kutoka kwa wazabuni.
- Kukusanya takwimu za kusaidia kutayarisha makisio ya vifaa vinavyohitajika na mpango wa Ununuzi (Procurement Plan).
- Kupokea vifaa ambavyo vimetumika lakini vinahitaji kutunzwa kabla ya kufutwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo.
- Kufungua na kutunza 'Bin Card' kwa kila kifaa kilichopo ghalani.
- Kufungua leja 'Ledger' ambayo itatunza kumbukumbu ya vifaa vinavyoingia kutunzwa na kutoka ghalani.
- Kukusanya na kutunza takwimu za wazabuni.
- Kukusanya na kutunza takwimu za upokeaji, utunzaji na usambazaji wa vifaa.
- Kupokea, kutunza na kusambaza vifaa
- Awe amehitimu Stashahada ya Afisa ugavi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

3. MSHAHARA

- Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali.

(C) USAFI WA MAZINGIRA 03.

1. Sifa za muombaji

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha Nne.
- Umri kuanzia miaka 18.
- Awe anajituma katika kufanya kazi bila kusimamiwa.
- Mwombaji awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu.

2. Kazi za Kufanya /Majukumu

- Kufanya usafi wa mazingira yanayozunguka maeneo ya Taasisi.
- Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.
2. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
3. Waombaji waambatinishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
4. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu.
5. Mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika, viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano na kudondoka au kupotea.
6. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingreza na yatumwe kupitia anuani ifuatayo;

Mkuu wa Taasisi,
Taasisi ya Sayansi za Afya Mbalizi,
S.L.P 6117,
Mbalizi – Mbeya.
Barua pepe: nursingmbalizi@yahoo.com
Namba ya Simu: 0762 939 181/0252 561 022/0762 351 978
Mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 24.01.2022 06:00 Mchana.

IMETOLEWA NA UONGOZI WA TAASISI YA SAYANSI ZA AFYA MBALIZI

SHUKRAN S. NDUMULLA
MKUU WA TAASISI.

TAASISI YA SAYANSI ZA AFYA MBALIZI

P.O BOX 6117
Mbeya
Tel. 025 2561022
Fax 025 2560348

P.O. BOX 6117
Mbeya
Tel. 025 2561023
Fax 025 2560348

Website :www.mbaliziinstitute.ac.tz Email :nursingmbalizi@yahoo.com

TANGAZO LA NAFASI YA UTOAJI HUDUMA YA CHAKULA KATIKA MGAHAWA (CAFTERIA) YA TAASISI YA SAYANSI ZA AFYA MBALIZI TAREHE 10.01.2022.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. **MWOMBAJI AWE NA LESENI YA BIASHARA.**
2. **MWOMBAJI AWE NA UZOEFU WA KAZI USIOPUNGUA MIAKA MIWILI.**
3. **MWOMBAJI AWE NA MPANGO MKAKATI WA UTOAJI HUDUMA YA CHAKULA.**

MWISHO WA MAOMBI NI TAREHE 24.01.2022 SAA 06:00 MCHANA.
MAOMBI YAPITIE KWA ANUANI IFUATAYO:

MKUU WA TAASISI,
TAASISI YA SAYANSI ZA AFYA MBALIZI,
S.L.P. 6117
MBEYA
BARUA PEPE: Email: nursingmbalizi@yahoo.com.
KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA: 0762 939 181/0762 351 978

TANGAZO HILI LIMEANDALIWA NA UTAWALA – MIHS

PRINCIPAL P.O. BOX 6117 MBEYA MBALIZI INSTITUTE OF HEALTH SCIENCES

SHUKRAN S. NDUMULLA.
MKUU WA TAASISI.